# KCSE NOV/DEC 2020 MOCK EXAMINATIONS

# 102/3 - KISWAHILI - Karatasi ya 3

## FASIHI

**Muda: Saa 2½**

**Jina............................................................ Nambari ya Mtahiniwa ..................**

**Sahihi.........................................................Tarehe:../12/2020 KIDATO 4...**

# KAPSABET HIGH SCHOOL

***Maagizo***

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali **manne** pekee.*
*(d) Swali la kwanza ni la **lazima.***
*(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani:Riwaya, Ushairi,Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi*
*(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.*
*(g) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(h) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizotengewa kwenye kijitabu hiki cha maswali.*
*(i) Kijitabu hiki kina kurasa **tano** zilizopigwa chapa.*
*(j) Mtahiniwa ni lazima ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa na maswali yote yamo.*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | | |

## SEHEMU A: TAMTHILIA
**P. Kea:** ***Kigogo***

1. **LAZIMA**

"...binadamu ni mavumbi na mavumbi atarejea kwa maana, kwa tamaa mtu anapenda kula kuku huku nduguze wakila kama kuku. Na katika uchu huo huo amependa kufikia kilele cha ufanisi kwa kukanyaga migongo ya wenziwe...

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

(b) Kwa kutoa mifano **mitatu** katika dondoo hili, ainisha taswira zinazojitokeza. (alama 6)

(c) Huku ukitoa mifano **kumi**, jadili namna Wanasagamoyo walilemaza juhudi zao za kujikomboa. (alama 10)

## SEHEMU B: RIWAYA
**Matei:** *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au 3*

2. "Barafu iliyokuwa imegandia moyoni ilianza kuyeyuka na moyo kutwaa uvuguvugu. Hatimaye uyabisi wa moyo wake ulitoweka."

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Taja na ueleze sifa sita za mrejelewa. (alama 6)

(c) Jadili maudhui yanayobainika katika dondoo hili. (alama 10)

**AU**

3. "Mama mtu alikuwa ameamua kwamba hapa hapamweki. Alikuwa amehudumu katika afisi za umma kama mhazili mwandamizi kwa miaka mingi mpaka kazi hii akaiona inamfanya kusinyaa, hana hamu tena."

(a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza riwaya ya Chozi la Heri. (alama 6)

(b) Huku ukitoa mifano jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa riwaya hii. (alama 14)

## SEHEMU C: USHAIRI

*Jibu swali la 4 au 5*

**4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ningeuzwa kuchaguwa, mambo nisiyo yapenda
Pasipo na kuchelewa, ningeanza na kukonda
Kujapo kwa kuuguwa, kunilaza kwa kitanda

Ningeishutumu njaa, kama adui mkuu
Aso na fao kufaa, mwana wala mjukuu
Mtu hapati kukaa, hatui ya juujuu.

Kisha ningetaja vita, nduli ya tangu zamani
Fundi wa vyembe na nyuta, si mwema simtamani
Ni mtu wa vutavuta, kamwa hapendi amani

Na katika mlolongo, kwenye huu msururu
Ningetaja na kifungo, kutokuwa na uhuru
Heri kwangu kuwa chongo, itakuwa haidhuru.

Kadhalika na ukata, ningasahau siwezi
Hauna pato kupata, kuyakidhi matumizi
Hana haramu mkata, dawamu ya muombezi

Ninguelani ukuwa, pamwe na athari zake
Nijapo kuvunjikiwa, ukanikuta upweke
Ni kama madhila huwa, una dhiki ndani yake

Na mishale kama hiyo, ifumayo moyo wangu
Inganipa jakamoyo, siyo matilaba yangu
Ngawa siridhiki kwayo, ni kudura zake Mungu

**Maswali**

(i) Eleza mambo ambayo nafsi neni hayapendi na kwa nini? (alama 5)

(ii) Kwa kurejelea shairi hili, eleza umuhimu wa: (alama 6)
- (a) inkisari
- (b) tabdila
- (c) kufinyanga sarufi

(iii) Ainisha bahari tatu za mashairi ukirejelea shairi hili. (alama 3)

(iv) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(v) Eleza mbinu tatu ambazo zimetumiwa kusanifu ubeti wa tatu. (alama 3)

**AU**

5. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Bustani za jadi
Maua ya kuchezea vipepeo
Na pua kufurahisha
Sasa ni mabaki ya kumbukumbu
Za yaliyojiri hapa
Na kukiacha kijiji kinywa wazi.

Hapa walimpiga mwereka
Dada yangu; mdogo wangu
Shuleni akitoka
Na mkoba wa kilo nzito za vitabu
Chini akakandamiziwa
Wakachana mbuga na wake ubikira!

Pale kando ya mto
Walimvizia na kumburura shangazi
Binamu zangu wadogo wakiona
Marinda wakamchania
Kabla ya kumtia kidonda shangazi
Naye ami kumchania kovu moyoni!

Ni hapa kando ya barabara kuu
Ambapo nyanyangu walimshika mkono
Uchochoroni wakamburuta
Na kumfanya kujutia
Bahati mbaya ya kuishi kwingi
Akaganda uchochoroni
Hadi alipoletwa nyumbani kesho yake
Na wachungaji wa machungani.

Si hapa walipomshurutisha mama
Chini wakamkanyagia
Kama kuku wa kuchinja
Baada ya yake sidiria kuikata?
Si hapa sebuleni mwetu?

Si hapa sokoni
Nilipopata vazi la stara
La wangu mke mpendwa
Lililokatwa yake mihimili?
Yule kichaa wa mwetu sokoni.
Akawa kichwani amelivaa
Na kuimba wimbo wa maombolezi
Huku wanakijiji wakimpuuza
Na watoto kumcheka?

Ni hapa ambapo usiku ulipoingia
Hawakusita kuhakikisha kuwa
Yule kichaa amawazalia mtoto
Na kujitia kundini kushangaa
Kilichomtuma atake kujifungua!

(*Timothy Arege)*

Maswali

(a) Tambulisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)
(b) Eleza dhamina ya mshairi. (alama2)
(c) Fafanua mbinu za kimtindo zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 5)
(d) Bainisha aina za taswira katika shairi hili. (alama 4)
(e) Onyesha toni ya mshairi. (alama 2)
(f) Onyesha matumizi ya mishata katika shairi hili. (alama 1)
(g) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

*Jibu swali la 6 au 7*

**A.Chokocho na D. Kayanda (Wah)**: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

6. ***D. Kayanda*: "Mwalimu Mstaafu"**

"Watu wa kwetu husema, 'Usilipe jema kwa baya', kwa hiyo mimi ninacho changu ambacho nitakupa kwa hiari yangu mwenyewe..."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) 'Usilipe jema kwa baya'. Fafanua kinaya katika kauli hii kwa kurejelea hadithi ya 'Mwalimu Mstaafu". (alama 16)

**AU**

7. ***Mtihani Wa Maisha (Eunice Kimaliro)***

(a) "Labda hata tayari ameona maajabu niliyoyafanya kwenye mtihani. Atanipa hongera kabla ya kunipa matokeo".

(i) Eleza mbinu kuu ya kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)

(ii) Fananua umuhimu wa msemaji wa dondoo hili ukirejelea hadithi ya "Mtihani wa Maisha". (alama 6)

**(b) *S. O. Hamad*: "Shibe Inatumaliza"**

"Ndugu yangu **<u>kula kunatumaliza</u>**."
"Kunatumaliza au tunakumaliza?"
Jadili ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kutoa mifano kwenye hadithi. (alama 12)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Kila kukicha mashaka
Ni kero hili si huba
Mimi pendo la viraka, heri demu la mkoba
Ingawa mno nataka, kuishi nawe muhiba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

Kamwe sitoshughulika
Nawaje wenye kuziba
Viumbe wanosifika, kwa fedha, chuma na shaba
Walostarabika, si mimi wa tobatoba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

Naapa sitojitweka
Limenichosha si haba
Nasomba vyangu viraka, nitie kwenye mkoba
Sikuye ya kuzinduka, mjinga hawi ni juba
Pendo viraka viraka
Litanishinda kuziba

(a) Huu ni wimbo wa mapenzi. Thibitisha. (alama 2)
(b) Eleza sifa <u>tatu</u> za nafsinenewa katika wimbo huu. (alama 3)
(c) Fafanua mbinu <u>nne</u> ambazo nafsineni ametumia kufanikisha uwasilishaji wake. (alama 4)
(d) Eleza faida <u>tano</u> za kurithisha wimbo huu kwa vizazi vijavyo. (alama 5)
(e) Unanuia kufanya utafiti kuhusu utungo wa maigizo:-
  (i) Eleza hatua <u>tatu</u> utakazofuata katika utafiti wa utungo huu. (alama 3)
  (ii) Fafanua udhaifu wa kuhifadhi utungo huu kwa njia ya maandishi. (alama 3)